JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OR- TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI LUPEMBE,
S. L. P. 114,
NJOMBE.
29/03/2022.

SIMU:
0756015658/0717015658 MKUU WA SHULE
0757172731/0628033907 MAKAMU MKUU WA SHULE
0754231771 TAALUMA
0753760283 MHASIBU
0688986642 PATRON
0766230585 PATRON
0743271823/0767261823 MALEZI

(Mawasiliano yote yaandikwe kwa mkuu wa shule na si mtu binafsi)
Unapojibu tafadhari taja:-

KUMB.NA.LSS/J.I/020/VOL.3/05
Ndugu……
Mzazi/Mlezi…….....

YAH: KUCHAGULUWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2022/2023

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka wa masomo **2022/2023** kwa tahasusi ya **CBG/EGM**.Shule ya sekondari Lupembe ipo umbali wa **kilometa 70** mashariki mwa mji wa Njombe, usafiri wa basi **Tsh.5,000/=** kutoka kituo cha mabasi Njombe mjini hadi mahali shule ilipo. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……** mwisho wa kuripoti ni tarehe **……..**

KAULI MBIU YA SHULE (SCHOOL MOTTO):*"ONE STEP DOES NOT MAKE A PATH".*

Kauli hii ndiyo dira yake kwa kipindi chote cha miaka miwili atakapokuwa hapa shuleni .Hivyo atatakiwa kuitafakari kauli hiyo na kuiishi kwa vitendo. Ni matumaini yetu kuwa atatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yake na kwa taifa kwa ujumla, atatakiwa kuwa na tabia njema , ahudhurie masomo siku zote na kujifunza kwa bidii.

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S.L.P 114
NJOMBE

KAZIULAYA A. J
(MKUU WA SHULE)

ADA MICHANGO MINGINE YA SHULE.

A. Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/=, mwanafunzi atalipa shilingi 35,000/= kwa muhula au ada yote kupitia akaunti namba **60601000014 NMB BANK** Jina la akaunti **LUPEMBE SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTI.** Tafadhari andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye pay in slip.Pindi afikapo shuleni aiwasilishe hati ya malipo kwa mhasibu wa shule.

B. Michango mingine inayotakiwa kulipwa na kila mzazi kwa mhula wa kwanza ni :-

i. 25,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani za shule.
ii. 6,000/=kwa ajili ya kitambulisho.
iii. 30,000/=kwa ajili ya taaluma(kwa mwaka).
iv. 12, 000/= kwa ajili ya umeme na maji.
v. 30,000/=kwa ajili ya walinzi na wapishi(kwa mwaka).
vi. 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza(kwa mwaka).
vii. 5,000/= kwa ajili ya tahadhari (haitarejeshwa).

Jumla ya Ada na michango mingine ni **Tsh.188,000/=(**kwa mwaka).

Tanibihi:Fedha zote zilipwe kupitia akaunti ya shule iliyo tajwa hapo juu na siyo kuleta fedha tasilimu(hazitapokelewa kabisa).

C. Mahitaji muhimu ambayo mwanao anapaswa kuleta shuleni ni :-

i. Ream ya karatasi 2 A4(kwa mwaka)
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika(orodha imeambatanishwa)
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa biology
iv. Scientific calculator original
v. Godoro la ft.$2^{1}/_{2}$
vi. Mashuka 2 rangi light blue,blanketi 1,chandarua,foronya na mto.
vii. Vyombo vya chakula(sahani,bakuli,kikombe na kijiko)
viii. Vifaa vya usafi na kazi za nje.
   - **CBG** Aje na Shoka lenye mpini, ndoo mbili kwa ajili ya usafi moja lita 20 nyingine ya lita 10.
   - **EGM** aje na panga, mopa, Ndoo mbili kwa ajili ya usafi moja lita 20 nyingine ya lita 10.
ix. Tochi kwa matumizi binafsi nyakati za usiku ni muhimu sana(ingawa umeme upo)
x. Aje na bima ya afya,cheti cha kuzaliwa na result slip pamoja na folder file moja.
xi. Madaftari makubwa 10 au zaidi ,pen, penseli,rula na mkebe.
xii. Toilet paper za kutosha muhula mzima.

SARE ZA SHULE

- Suruali 2 rangi ya kijivu mpauko zenye mifuko 2 mbele na 1 nyuma, upana miguu.
- inch.18, makoti 2 rangi kijivu(suti) pamoja na tai rangi nyeusi.
- T-shirt2 za rangi ya kijivu mpauko zenye kola(form six)
- Sweta 2 rangi ya kijani jeshi.
- Track suit rangi kijivu.
- Mashati meupe 2 ya mikono mirefu.
- Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 vya kufunga na kamba visivyo na visigino virefu.
- Raba/viatu , jezi nyekundu isiyo na maandishi na track suit rangi nyekundu kwa ajili ya michezo(muhimu sana)
- Soksi jozi 4 au zaidi rangi nyeusi na soksi nyekundu za michezo pair 1.
- Koti jeupe lenye mikono mirefu (laboratory coat) kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi tu.
- Suruali nyeusi 2 za kitambaa, ambayo ni sare ya kazi baada ya masomo.Aidha mshono ufanane na sare ya darasani.

Tanibihi:

1. Kuepusha usumbufu vitu vifuatavyo vinapatikana mazingira jirani na shule; (Tshirt kijivu, Tai, sweta, nguo za michezo, mashati meupe ya shule, soksi nyeusi, raba za michezo, mashuka)
2. Mwanafunzi anapokuja shuleni aje akiwa amevaa T-shirt na track suit ya kijivu kama ulivyoelekezwa hapo juu.Pia mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za aina nyingine zaidi ya hizo zilizoelekezwa.

USAFI BINAFSI

Mwanafunzi anatakiwa kuja shuleni na nywele fupi,asinyoe panki au upala,haruhusiwi kufuga ndevu wala kucha, aoge mara kwa mara na kutunza mazingira ya shule.

USHIRIKI WA KAZI ZA MIKONO.

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kazi za mikono ambazo zina lengo la kuendeleza Elimu ya Kujitegemea (E.K) pamoja na kuimarisha afya ya mwili.

NIDHAMU.

Ili mwanafunzi aweze kujifunza na kufaulu katika masomo yake atatakiwakuwa na nidhamu ya hali ya juu.Unatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sheria za shule zilizo ambatanishwa kwenye fomu hii.Pia ifahamike kuwa si jukumu la shule kutoa nauli pindi mwanafunzi anapopatikana na makosa ya kinidhamu ya kumrudisha nyumbani.Ni wajibu wako mzazi/mlezi.

MICHEZO NA UTAMADUNI.

Kila mwanafunzi atatakiwa kushiriki michezo na utamaduni kwa lengo la kuleta uhusiano mwema na kujenga afya ya mwili.Mwanafunzi ajitokeze na kuibua kipaji chake katika fani mbalimbali mfano ;mpira, kuimba, kuigiza ,skauti nk.

DINI

Kila mwanafunzi anaruhusiwa kufanya ibada kulingana na imani yake ili mradi shughuli hizo zitaendeshwa kufuatana na sheria za nchi, sheria, kanuni, taratibu na ratiba ya shule.Aidha mwanafunzi atasali/swali shuleni au maeneo mengine kama atakavyoelekezwa na shule na si vinginevyo.

CHAKULA MAALUMU.

Shule haitatoa chakula maalumu kwa wanafunzi tofauti na wengine.Aidha mzazi/mlezi unashauriwa kumtafutia mwanao mahali ambapo ataweza kusoma na kupata huduma ya chakula kulingana na tatizo lake.Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja

LUPEMBE SEKONDARI.
KARIBU SANA.
MKUU WA SHULE.

NAKALA;

1. **KATIBU MKUU,**
   OFISI YA RAIS-TAMISEMI,
   S. L. P. 1923,
   DODOMA

2. **KATIBU TAWALA MKOA,**
   S.L. P. 668,
   NJOMBE.

3. **MKURUGENZI MTENDAJI(W),**
   S. L. P .547,
   NJOMBE.

SHULE YA SEKONDARI LUPEMBE

SHERIA ZA SHULE.

1. Wanafunzi wanatakiwa kusimama kumsalimu mtu yeyote anaye wazidi umri anapopita,anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mkutano.
2. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimiana na kuwa na ushirikiano .
3. Wanafunzi wanatakiwa na kufanya kazi wanazopewa
4. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
5. Wanafunzi kuwa mfano mwema ndani na nje ya shule.
6. Wanafunzi waheshimu ofisi ya mkuu wa shule, ukumbi wa chakula ,maktaba, na madarasa.
7. Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria masomo kwa wakati na kufanya mitihani yote inayowahusu na kama kuna sababu ya kutohudhuria ielezwe mapema.
8. Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria na kufanya kazi za mikono watakazopangiwa.
9. Wanafunzi wanatakiwa kuwa katika mikusanyiko yote kama ;kupandisha Bendera ya Taifa, Baraza la shule na mikutano ya darasa au bweni.
10. Wanafunzi wanatakiwa kutii kengele kama mwito wa haraka.
11. Wanafunzi wanatakiwa kuwa shuleni, shule inapofunguliwa kwa tarehe iliyopangwa.
12. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare za shule:-darasani, wanapotoka nje ya shule,wakati wa baraza la shule.
13. Wanafunzi watatoka nje ya shule kama wana shida binafsi kwa ruhusa ya :- mwalimu wa zamu,au mkuu wa shule tu kama ni kulala nje ya shule.

Tanibihi:

MWANAFUNZI AKILALA NJE YA SHULE BILA RUHUSA ATAKUWA AMEJIFUKUZISHA SHULE MWANYEWE.

14. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea nyumba za walimu na watumishi wengine,sehemu hizi ni nje ya mipaka ya shule.
15. Wanafunzi hawana ruhusa ya kuingiza mgeni yeyote bwenini au madarasani.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea au kujihusisha na maeneo yafuatayo:- vilabu vya pombe, majumba ya starehe au ya kufukia wageni (guest houses).
17. Mwanafunzi anatakiwa :- kutunza mali ya uma kama madawati, viti, vitanda, majembe, slasher, ndoo, vifaa vya kulia chakula, vioo vya madirisha, vitabu, vifaa vya maabara, mali binafsi nk.pamoja na kulala bwenini wakati wote anapokuwa shuleni.
18. Wanafunzi wanatakiwa kuwa wasafi binafsi na kutunza mazingira ya shule.
19. Wanafunzi hawaruhusiwi kuwa na jiko, heater, simu na vifaa vingine vinavyotumia umeme.

20.Mwanafunzi hatakiwi kuvaa nguo za nyumbani(mwanafunzi atavaa shamba dress
muda ambao sio wa masomo)
21.Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa **mikufu , shanga, hereni**, au **bangili.**

MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi
2. Uvutaji sigara na bangi
3. Kupigana au kumpiga mwanafunzi,mwalimu au mtumishi.
4. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa(mahusiano ya kimapenzi)
5. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
6. Kutoa mimba/kusaidia kutoa mimba.
7. Kutoa lugha chafu/matusi kwa mwanafunzi, kwa mwalimu au kwa mtumishi mwingine.
8. Kupatikana na makosa ya jinai.
9. Kugoma na kuchochea au kuongoza mgomo shuleni.
10. Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
11. Kutohudhuria masomo kwa siku 90 au zaidi bila taarifa/utoro.
12. Kupatikana na simu, vifaa vyake au vyote kwa pamoja.
13. Kupatikana na kondomu.
14. Kutoroka mchana au usiku.
15. Kuchezea miundombinu mathalani ya umeme, maji, vyoo nk.
16. Kufuga ndevu.
17. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
18. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za shule.
19. Kufanya jaribio lolote la kujiua/kuua mfano kunywa sumu nk.
20. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
21. Kuhubiri dini, siasa au jambo lolote lenye kuhatarisha amani au usalama wa shule na nchi kwa ujumla.Sala/ swala zote zifanyike wakati uliopangwa na sehemu sahihi kulingana na maelekezo ya shule.

Tanibihi:Soma kwa makini maelezo/maagizo/sheria za shule na kutekeleza kikamilifu.

“KARIBU SANA LUPEMBE SEKONDARI”

.....

KAZIULAYA A. J

(MKUU WA SHULE)

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S.L.P 114
NJOMBE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI:
1.Jina la mwanafunzi…….
2.Tarehe ya kuzaliwa……
3.Mahali alipozaliwa(wilaya)……..(mkoa)……
4.Dini……....Dhehebu…….

1.Jina la mzazi/mlezi anayekutunza…….
2.Kazi ya mzazi/mlezi……..
3.Anwani ya mzazi/mlezi…….
4.Mahali anapoishi mzazi/mlezi:-mkoa……wilaya…….
Kijiji/mji……kata……..

1.Jina la anaye kulipia ada ya shule…….....uhusiano……
2.Anwani yake…….
3.Namba ya simu……..

Anwani za ofisi ya katibu kata au mwenyekiti wa mtaa/kijiji ambako mzazi/mlezi wa mwanafunzi
anaishi:-
1.Jina la Afisa kata……..
2.Kata ya……
3.Anwani…….
4.Namba ya simu…….

1.Jina la mwenyekiti wa kijiji/mtaa…….....
2.Kijiji/mtaa wa ……
3.Anwani……
4.Namba ya simu……

1.Jina la ndugu wa karibu…….....
2.Kijiji/mtaa wa ……
3.Anwani……
4.Namba zake za simu……

Tanibihi:-**Fomu hii ijazwe kwa uangalifu na taarifa ziwe sahihi**.

FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI.

I. MWANAFUNZI

Mimi…….kidato ……. Nakubali kujiunga na shule hii ya sekondari Lupembe nikiwa mwanafunzi wa Bweni.Nimesoma na kuyaelewa maelezo yote, sheria na taratibu zote za shule.Ninakubali kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Lupembe.Kwa hiyo ninaahidi kwamba :-

1.Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.
2.Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vile ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa chama tawala na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
3.Nitatunza mali ya uma ambayo ni pamoja na mazingira, samani, vitabu nk.
4.Nitasoma kwa bidii na juhudi ili nifaulu.
5.Nitashiriki katika shughuli nyingine za nje mbali na masomo ya darasani.

Sahihi ya mwanafunzi……. Tarehe……

II. MZAZI/MLEZI:

Mimi……..ninakubali mtoto wangu……..... kujiunga shule ya sekondari Lupembe kidato……mwaka 2022/2023 tarehe…….akiwa mwanafunzi wa bweni.Kwa hiyo naahidi kwamba :-

1.Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule, walimu na wafanyakazi wengine wa shule katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu.Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.
2.Nitafanya kila niwezalo ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema, kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufaulukwa muda wote awapo shuleni.

Anwani yangu ya kudumu ni ……
Namba ya simu ya mzazi/mlezi……. Email……
Sahihi ya mzazi/mlezi……..……tarehe……..

III:KUWATEMBELEA WANAFUNZI/SIKU YA WAGENI

Wazazi/walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa mwezi ambayo ni kila Jumapili ya kwanza ya mwezi kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 10:30 jioni.Mwalimu wa zamu atakuwepo shuleni kwa muda huo kupokea wageni.Hairuhusiwi kumletea mwanafunzi chakula

FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

LUPEMBE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX. 114,
NJOMBE.
DATE:……

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S.L.P 114
NJOMBE

THE MEDICAL OFFICER:
……..
……
……

RE:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION
To be completed by a medical officer in respect of all form five students

Full name…….age……..…….years. Sex…….

1. Blood count(red and white)……...
2. Stool examination……...…
3. Urine analysis……
4. Eye test……..
5. T.B test……..……
6. Ears……
7. Chest……..
8. Spleen……
9. Abdomen……..……
10. ADDITIONAL INFORMATION eg. Physical defects or important infections, chronicof family diseases etc.
    ……
    ……
    ……
    ……

11. General comments:-

……
……
……
……

SIGNATURE…… DATE……...….STAMP……

ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILASOMO

A: **CHEMISTRY**

- Advanced chemistry Review by Willam W Davis(Mzumbe bookshop project 2004)
- Physical chemistry by Delungu et(Mzumbe bookshop project 1998)
- Advanced level in organic chemistry part I and II(TIE 1995)
- Organic chemistry volume I.The fundamental principles by I.L Finar(Longman Ltd 1990)
- NGAIZA'S SERIES OF ADVANCED CHEMISTRY PHYSICAL CHEMISTRY 2014
- NGAIZA'S SERIES OF ADVANCED CHEMISTRY ORGANIC CHEMISTRY 2014
- NGAIZA'S SERIES OF ADVANCED CHEMISTRY INORGANIC CHEMISTRY 2014

B: **BIOLOGY**

- New understanding Biology by Suzan Toole
- Advanced biology by Michael Kent
- Biological science third by D.J.Tylor, N.P.O Green and G.W.Stout
- Advanced biology principle and applicationby C.J.Clegg and D.G.McKean
- New understanding biology for advanced level by Glenn and Suzan Toole
- Plant and animal biology vol.1&2 by A.E. Vines and N.Rees
- Biology for class XI&XII by Dr.P.S.Verma and Dr. B.P.Pandey
- Biological science by CHANDS
- Biology by Msaki series (classification, genetics and cytology)

C**: GEOGRAPHY**

- Principle of physical geography by F.J.Monkhouse
- Geography;Integrated Approach by D.Waugh
- Practical geography for Africa by J.M.Pritchard
- General geography in diagram by R.B.Bunnert
- Essentials of Practical Geography by Josephat Mwita
- Simplified physical geography(A level) by D.M
- Statistical methods and the geographers
- Human and Economic Geography by Morgan goh cheng leong

D: ADVANCED MATHEMATICS.

- CHANDI I & II
- BACKHOUSE I & II
- PURE MATHEMATICS I & II
- UNDERSTANDING ADVANCED MATHEMATICS
- ENGENEERING MATHEMATICS
- PURE MATHEMATICS (TRANTER)
- REVIEWS ADVANCED MATHEMATICS 1 & 2
- KINUNDA
- UNDERSTANDING MATHEMATICS

D: **BASIC APPLIED MATHEMATICS**

- Basic Applied Mathematics by Kiza and Septine I.Sillem

- Basic Applied Mathematics by TIE
- Pure mathematics I&II by Bank house
- Core course Mathematics by Bostoch and Chandler

E:ECONOMICS

- AMBILIKILE – NEW SYLLABAS -2009
- MORDEN ECONOMIC –ROBERT MUDIDA
- ECONOMIC 1 ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010 SYLLABUS
- ECONOMIC 1I ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010 SYLLABUS
- ECONOMIC A/LEVEL PAPER 1 AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M.AMBIKILE NEW SYLABUS
- ECONOMIC A/LEVEL PAPER 1I AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M.AMBIKILE NEW SYLABUS

F: **GENERAL STUDIES**

- General studies for A-Level certificate form v
- Contemporary approach for A-level general studies notes for form five and six
- General studies supplementary book for A level and colleges
- Advanced level general studies notes for form 5 and 6 by Nyambari Nyangwine 2009
- General studies for A-Level certificate form v and vi by Richard R.F.

NB

MWANAFUNZI LAZIMA AWE NA KITABU KIMOJAWAPO KWA KILA SOMO LA TAHASUSI YAKE.

RANGI YA SWETA **RANGI YA SUTI**

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S.L.P 114
NJOMBE